# MAKUBALIANO

yanayotajwa hapa kama “Makubaliano’ baina ya (Kwamtili Estate Ltd) Shamba la Kwamtili, Sanduku la posta 120, Tanga, kampuni iliyosajiliwa, inayojulikana kama (Kwamtili Estate) “Shamba la Kwamtili”, na (Kwamtili Group) Kikundi cha Kwatili, kilicho Kwamtili, Wilaya ya Mkinga, inayotajwa hapa kama “Kwamtili Group”, kikundi cha watu binafsi, walioorodheshwa kwa kiambatisho cha Makubaliano haya (wa Makubaliano haya kwa kukubali kusimamia, kutengeneza na kuuza kakao inayotoka kwa miliki zilizomilikiwa na Shamba la Kwamtili, katika wilaya ya Mkinga inayotajwa hapa kama “Shamba”.

**1. Upeo wa Makubaliano haya:**

Upeo wa Mkataba huu unajumuisha shughuli zifuatazo zitakazokamilishwa na Kikundi cha Kwamtili:

- kushughulika na taratibu za kilimo zinazohitajika kwa uzalishaji wa kakao katika miti iliyopo katika Shamba ili kuhakikisha uzalishaji wa mazao yenye ubora wa kiwango cha juu kabisa;
- Kuanzisha, baada ya makubaliano na Shamba la Kwamtili, vitalu vya kakao katika sehemu zilizoteuliwa katika maeneo ya Shamba;
- kuotesha , kwa makubaliano na Shamba la Kwamtili, niti mipya ya mikakao kwa sehemu zilizoteuliwa katika Shamba;
- kuvuna, kutengeneza, kukausha, kupanga viwango, na kuhifadhi kakao kwa ajili ya kuuzwa na, Kikundi cha Kwamtili wakitumia vifaa vilivyotolewa na Shamba la Kwamtili;
- kutoa ulinzi kwa Shamba nzima kwa mujibu wa orodha iliyokubalika ( inayotajwa hapa kama “Orodha” ya vitu vilivyokubalika), ilivyoambatishwa katika Makubaliano haya yanajyojumisha maeneo ya msitu, maeneo yanayolimwa na wakulima kwa mkataba, maeneo yeneye miti ya mikakao, majengo, kiwanda, miundombinu na vitu vingine vilivyoorodheshwa na Kwamtili katika orodha iliyotajwa hapo juu ambayo itakamishwa na kuwekwa saini ya mwisho makubaliano haya;
- kudumisha katika utaratibu mzuri, vitu vyote vilivyobainishwa katika Orodha hii.

**2. Muda wa Makubaliano**

Makubaliano haya yatakuwa ni kwa muda wa mwaka mmoja (1) na kaweza kurejewa tena kwa vipindi vya mwaka mmoja mmoja baadaye.

Kwa kawaida makubaliano haya yataanza tarehe mosi(1) mwenzi wa Januari na kuishia tarehe 31 ya mwezi wa Desemba kila mwaka.

Hata hivyo wadau wanaweza kuingia katika makubaliano mwanzo wa miezi ya nje ya kipindi cha kuvuna kakao iliyoanishwa kama Octoba, Novemba na Desemba, na Mei Juni na Julai.

**3. Ad**

Ili kupata ruhusa ya kuvuna,kutengeneza na kuuza kakao, Kikundi cha Kwamtili kitalipa ada ya kila mwaka TZS1____,000 ( shilingi laki ____ ya Tanzania) kwa Shamba la Kwamtili.

Ada lazima ilipwe kabla ya kujiunga na/au kufanya upya Makubaliano haya na ilipwe pesa taslimu kwa mwakilishi aliyeteuliwa wa Kwamtili Estate au kupitia akaunti ya benki.

**4. Wajibu wa kikundi cha Kwamtili**

Kikundi cha Kwamtili kitawajibika:

- kubeba gharama zote za miche,mbolea,wafanya kazi,chemikali,dawa ya kuulia wadudu,zana na mashine kwa ujumla zinazohitajika kutunzia kakao na kwa kutengeneza, kukausha, kusafirisha na kuhifadhi kakao;

- kweka ulinzi wa shamba nzima kwa mujibu wa orodha, kulinda dhidi ya wizi, uchomaji moto na shughuli nyingine ambazo zinaharibu ustawi wa Shamba pamoja na uvamizi, ukataji wa miti, ufyekaji wa shamba na sehemu zenye misitu na uharibifu wa makaazi na njia za maji;

- kutunza zana zote na vitu vyote vinavyotajwa katika orodha viko katika hali nzuri ya kutumika;

- kutoa taarifa ya utekelezaji wa masuala yote ya majukumu ya Kikundi cha Kwamtili kila baada ya wiki mbili kwa mwakilishi aliyeteuliwa wa Shamba la Kwamtili. Itatolewa taarifa ya mdomo kutoka kwa wanachama wasiopungua wane (4) wa Kikundi cha Kwamtili akiwemo mwenyekiti wa Kikundi cha Kwamtili. Saa, tarehe na mahali pa kila kikao cha kupena taarifa itaainishwa kwenye kikao cha nyuma yake, na kikao cha kwanza kila mwaka itapangw na pande zote mbili kabla ya kutia saini mkataba na si zaidi ya mwezi mmoja baada ya kutia saini ya mwisho ya mkataba.

**5. Majukumu ya Kwamtili Estate**

Shamba la Kwamtili:

- Itakipatia Kikundi cha Kwamtili ruhusa, isiyo na vikwazo, ya kutembelea maeneo ya Shamba ambayo yameteuliwa kama vitalu au maeneo ya kukuzia kakao.

- Itakipatia Kikundi cha Kwamtili ruhusa, isiyo na vikwazo, ya kutumia majengo, kiwanda, mashine kwa ujumla na zana za kufanyia kazi ambazo zimebainishwa katika Orodha;

- itakubali kwa busara uchakavu wa majengo, kiwanda, mashine kwa ujumla na zana zilizotajwa kwenye Orodha lakini bila jukumu ya kukarabati au kubadilisha majengo, kiwanda, mashine kwa ujumla na zana zilizotajwa katika Orodha zilizoharibika, zisizorekebishika au zisizokuwepo.

**6. Masharti kwa Jumla**

Kwa malengo ya kutekeleza Makubaliano haya:

- Mawasiliano yote, lazima yatumwe kwa mkaguzi wa Shamba la Kwamtili au kwa mtu mwingine aliyeteuliwa kwa maandishi na Bw Dennis Fielder, Mkurugenzi Mtendaji, wa Shamba la Kwamtili, au warithi wake kama mshiriki mkuu mwenye hisa nyingi zaidi;

- Maelekezo pekee ambayo Kikundi cha Kwamtili kitafuata ni yale yaliyotolewa na mtu aliyeteuliwa kwa maandishi na Bw Dennis Fielder, Mkurugenzi Mtendaji, Shamba la Kwamtili, au warithi wake kama mshiriki mkuu mwenye hisa nyingi zaidi;

- Kikundi cha Kwamtili kitawajibika kwa ushuru wote na kodi zote za serikali zinazohusiana na mwenendo wa shughuli zilizotajwa katika Makubaliano haya;

- mbali na taarifa inayotolewa kila baada ya wiki mbili, Kwamtili Estate itafanya ukaguzi kila mwaka kwa Orodha inayokwenda na wakati ndani ya mwezi mmoja wa makamilisho ya mwaka na saini ya Makubaliano haya ili kurekebisha hali iliyopo ya vitu vilivyoorodheshwa.

**7. Katiba ya Kwamtili Group**

Kwamtili Group itaanzishwa kama ifuatavyo:

- Orodha ya watu binafsi wanaohusika na Kikundi cha Kwamtili, wakiwa kikundi cha watu binafsi walioorodheshwa katika kiambatisho cha Makubaliano haya, itaanzishwa kabla ya saini ya Makubaliano haya ya mwisho;

- Idadi ya watu binafsi ambao ni wanachama wa Kikundi cha Kwamtili haitazidi watu kumi na watano(15) waliotajwa;

- Kwamtili Group itakuwa na Mwenyekiti, Mshika Fedha na Katibu waliochaguliwa kihalali kama maafisa kutoka miongoni wa wanachama walioteuliwa katika kiambatisho cha Makubaliano haya;

- Mabadiliko katika orodha ya wanachama na mabadiliko ya maafisa waliochaguliwa lazima yajulishwe, kwa maandishi, kwa Shamba la Kwamtili. Kikundi cha Kwamtili lazima kitoe ushahidi kwa maandishi kwamba uchaguzi wa maafisa umeshafanyika kufuatana na kanuni zilizowekwa na Serikali ya Tanzania ili kudhibitisha vikundi vilivyoandikishwa;

- uchaguzi lazima ufanyike kila mwaka na maafisa a) wachaguliwe kwa kiwango kisichozidi mihula mitatu mfululizo na b) wawe na haki ya kurejea tena katika uchaguzi baada ya muda wa mwaka mmoja;

- Wanachama wote wa Kikundi cha Kwamtili watakuwa na majukumu na wajibu sawa, kila mmoja akifanya kazi kwa kiwango muhimu ili kudumisha maeneo ya kukuza kakao;

**8. Kuvunja Makubaliano**

Makubaliano haya yanaweza kuvunjwa wakati wowote kwa maandishi na Shamba la Kwamtili kama:

- Kwamtili Group ikifanya shughuli yoyote ile katika Shamba, ambayo haikutajwa na masharti ya Makubaliano haya, au ni kinyume cha sheria kwa asili au haikuidhinishwa kwa maandishi kutoka kwa mwakilishi mteule wa Shamba la Kwamtili au Mkurugenzi Mtendaji au warithi wake;

- Kwamtili Group haikamilishi wajibu wake wa kutunza mikakao na vifaa vya uzalishaji wa kakao na vitendea kazi katika hali nzuri na kutoa ulinzi na kuzuia uharibifu wa kipengele chochote cha Shamba;

Makubaliano yanaweza kusitishwa na upande mmojawapo kwa kutoa ilani isiyopungua miezi mitatu (3) kwa maandishi kwa upande mwingine, kwa wakati huo pande zote mbili zitafanya

mapitio taratibu ya mali zilizomo katika Orodha. Upotevu wowote au ushukaji wa thamani uliyozidi uharibifu na uchakavu unaokubalika lazima urekebishwe na Kikundi cha Kwamtili.

Kutokana na kuvunjwa kwa Makubaliano, kakao yote iliyokamilika kutengenezwa katika hifadhi inaweza kutolewa kutoka kwa shamba na Kikundi cha Kwamtili.

**9. Dhamira ya nia njema**

Pande zote mbili zimekubali kufanya kazi kwa amani kuelekea kwenye mafanikio ya utekelezaji wa Makubaliano haya na wanaelezea makusudio ya kutatua kwa njia ya amani hali yoyote ya kutoelewana juu ya tafsiri ya kifungu chochote au hali yoyote itakayojitokeza katika utekelezaji wa Makubaliano.

Makubaliano haya yataanza kufanya kazi tarehe: ............................

Sahihi:

| | |
|---|---|
| ................................. | ................................ |
| Mkurugenzi Mtendaji | Mwenyekiti |
| Shamba la Kwamtili | Kikundi cha Kwamtili |
| Tarehe:.................................. | Tarehe:....................... |

**<u>Kiambatisho:Kikundi cha Kwamtili</u>**

<u>Wanachama</u> (jina na kijiji cha makaazi)

<u>Maafisa</u> ( jina, kijiji cha makaazi , na tarehe ya uchaguzi:

| | |
|---|---|
| Mwenyekiti: | ..................................................... |
| Katibu | ..................................................... |
| Mshika Fedha: | ..................................................... |

**<u>Kiambatisho: Shamba la Kwamtili – Orodha ya vifaa vilivyokubalika</u>**